

# Zab. 127

M: Jeannot Amani Mulume

♩ = 70

Bwa - na a - tu - ba - ri - ki - e si - si si - ku zo - te za ma - i - sha ye - tu.

5 Sib Ré m Mib Fa4-3 Sib Ré m7 Sol m Mib Dom Fa9/4--3

## MASHAIRI:

1. Heri mtu anayemheshimu **Bwana**  
Anayeenda katika njia **zake!**  
Kwa taabu ya mikono ya **ko** utashiba,  
Utaona heri na **raha.**
2. Mke wako kama mzabibu **mzazi**  
Ndani ya nyumba **yako;**  
Waana wako kama **miche** ya mizeituni,  
Wakizunguka meza **yako.**
3. Ndivyo anavyobarikiwa, mtu mwenye kumheshimu **Bwana!**  
Bwana akubariki toka **Sioni:**  
Uone usitawi wa Yerusalemu  
Siku **zote** za maisha **yako!**